



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
TAASISI YA UTAFITI WA MISITU TANZANIA



AGOSTI 7, 2019

TANGAZO

UUZAJI WA MITI AINA YA VITEX (*VITEX KINENSIS*) KWA NJIA YA MNADA ILYOPO KATIKA KISHAMBA CHA UTAFITI LUSHOTO, TANGA.

1. Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) inatarajia kuuza jumla ya miti 397 aina ya Vitex (*Vitex kinensis*) yenye kipenyo kati ya 15cm – 51cm na jumla ya mita za ujazo **415.9488** iliyopo Lushoto. Mauzo haya yatafanyika tarehe **19 Agosti, 2019** katika Kituo cha Utafiti wa Misitu – Lushoto saa **tano (5:00) asubuhi**. Uuzaji utafanyika kwa njia ya mnada kwa kuzingatia Kanuni 31 (ii) ya kanuni za sheria ya misitu za mwaka 2004. Miti hii ya vitex itauzwa mahali ilipo na jinsi ilivyo na mnunuzi hatakuwa na haki ya kudai fidia baada ya mauzo.
2. Kampuni au mtu binafsi anayetaka kushiriki mauzo haya kwa njia ya mnada anatakiwa kuwasilisha barua ya maombi kwenye bahasha iliyofungwa na juu yake kuandikwa MNADA WA MITI, kuonesha nia ya kushiriki mauzo kwa njia ya mnada akiambatanisha leseni ya biashara, usajili wa biashara ya mazao ya misitu (logs/timber) (2018/19) na cheti cha utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN).
3. Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania inawaalika wenye nia ya kushiriki mnada kutuma maombi yao kwa anuani ifuatayo: **Mkurugenzi Mkuu, TAFORI, S. L. P. 1854 MOROGORO**. Mnunuzi atatakiwa kuonesha katika maombi yake bei ya jumla ya kununua miti kama ilivyoainishwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 1: IDADI YA MITI NA BEI YA AWALI

Aina ya miti	Idadi ya Miti	Jumla ya Ujazo (Meta za Ujazo)	Bei ya Awali (Tshs)
Vitex (<i>Vitex kinensis</i>)	397	415.9488	50,558,576.64

- Izingatiwe kwamba, bei ya juu itakayotolewa na mnunuzi wakati wa kufungua bahasha haitazuia wanunuzi wengine waliowasilisha maombi au yeye mwenyewe kuongeza bei zaidi ya iliyotajwa awali.
- Mnada utaendeshwa hadharani wakiwepo wanunuzi wote katika Kituo cha Utafiti wa Misitu - Lushoto siku ya **Jumatatu 19 Agosti 2019**. Mnada utaendeshwa kwa kufuata sheria ya misitu sura ya 323.
- Mnunuzi atakayefanikiwa kununua miti ya Vitex katika mnada huu hataruhusiwa kusafirisha magogo nje ya nchi kwa mujibu wa kanuni ya 50(1) ya mwaka 2004. Kusafirisha Mazao nje ya nchi ni baada ya kuyachakata kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na 69 la Mwaka 2006.
- Mnunuzi atakayefanikiwa kununua miti ya Vitex katika mnada huu atawajibika kuchukua hati ya malipo (Bill) pamoja na masharti ya uvunaji toka Ofisi ya TAFORI Lushoto.
- Makampuni na Watu binafsi wanakaribishwa kutembelea eneo la miti inayouzwa wakati wa saa za kazi kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi mpaka saa tisa (9:00) alasiri. Mkurugenzi wa Kituo au Afisa aliyeteuliwa atakuwepo kwa ajili ya maelezo zaidi.

9. Bei ya miti ya Vitex iliyooneshwa katika Jedwali Na 1 inajumuisha malipo yote yaani ‘VAT’, CESS, FOREST ROYALTY, na LMDA.
10. Mnunuzi atakayeshinda atalipa asilimia ishirini na tano (25%) ya jumla kuu na kuwasilisha nakala ya hati ya malipo (Bank Pay In Slip) ndani ya siku tatu za kazi, fedha hizo hazitarudishwa. Asilimia sabini na tano (75%) iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya mnada. Malipo yote yatafanyika kwa kupitia akaunti ya Taasisi kama ifuatavyo:

Jina la Akaunti: TAFORI GENERAL ACCOUNT

Namba ya Akaunti: 22101100006

Bank: NMB

11. Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Taasisi **www.tafari.or.tz**
12. Mnunuzi atatakiwa kuondoa mazao ya misitu aliyonunua ndani ya mwezi mmoja baada ya kumaliza kulipa malipo yote kwa asilimia mia moja (100%)
13. Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Ijumaa, **tarehe 16 Agosti 2019 saa tisa (9:00) mchana**. Wanunuzi watakaochelewa kuwasilisha maombi yao kwa siku na muda uliopangwa hawataruhusiwa kushiriki katika majadiliano ya mauzo.

Imetolewa na

Kaimu Mkurugenzi Mkuu,

Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI)